



KWA AJILI YA VIJANA

Mungu Hana Ubaguzi

Maagizo: Fanya zoezi hili katika mazingira matulivu. Unaposoma maandiko, jiwazie ukiwa katika matukio yanayozungumziwa. Wazia kikao. Sikia sauti. Hisi kama wahusika wanavyohisi. Wazia kwamba masimulizi haya ni halisi kabisa.

Wahusika wakuu: Kornelio, Petro

Kwa ufupi: Petro anaiga sifa ya Mungu ya kutokuwa na ubaguzi kwa kumhubiria Kornelio ambaye si Myahudi.

1 CHUNGUZA TUKIO HILI.—SOMA MATENDO 10:1-35, 44-48.

Wazia na ueleze jinsi Kornelio anavyoonekana. _____

Unafikiri Kornelio alihisi jinsi gani alipozungumza na malaika, kama mstari wa 3 hadi 6 unavyotaja? _____

Unafikiri Kornelio na watumishi wake walizungumzia nini kama inavyodokezwa katika mstari wa 7 na wa 8? _____

2 CHIMBA ZAIDI.

Kwa nini mfano ambao Petro alionyeshwa katika mstari wa 10 hadi 16 ulikuwa na matokeo? (Dokezo: Fikiria malezi ya Petro akiwa Myahudi, kama mstari wa 14 unavyodokeza.) _____

Unatambua sifa gani ya Kornelio katika mstari wa 25? Kwa nini si jambo la kawaida kwa mtu mwenye cheo kama chake kuwa na sifa hiyo? (Dokezo: Ona mstari wa 1.) _____

Kwa kutumia vifaa vya utafiti unavyoweza kupata, chunguza hesabu ya wanajeshi katika kikosi cha Italia ambacho Kornelio alisimamia. _____

Kwa nini kugeuzwa imani kwa Kornelio ni jambo la maana sana? _____

3 TUMIA MAMBO ULIYOJIFUNZA. ANDIKA MAMBO ULIYOJIFUNZA KUHUSU . . .

Kutumia mifano kwa njia yenye matokeo. _____

Sifa ya Mungu ya kutokuwa na ubaguzi. _____

Jinsi unavyoweza kuonyesha sifa hiyo ya kutokuwa na ubaguzi. _____

4 NI JAMBO GANI KATIKA SIMULIZI HILI AMBALO LIMEKUGUSA MOYO SANA, NA KWA NINI?

